

MWONGOZO

**MTIHANI WA PAMOJA WA ROYAL**

Kenya Certificate of Secondary Education



**102/1 — KISWAHILI — Kartasi ya 1**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**1. SWALI LA LAZIMA**

Andika barua kwa waziri wa kilimo kupitia kwa katibu wa kilimo huku ukipendekeza jinsi nchi ya Kenya inavyoweza kukabiliana na janga la njaa.

Insha izingatie

- Hii ni barua rasmi
- Iwe na muundo ufuatao

Anwani ya mwandishi

Anwani ya mwandikiwa

Kupitia kwa anwani ya katibu wa kilimo

Kwa Bwana/Bi

**YAH: MAPENDEKEZO YA KUKABILIANA NA JANGA LA NJAA**

Hoja

- Kuhifadhi maji wakati wa mvua ili kutumika nyakati za kiangazi.
- Wananchi kufunzwa namna ya kuzingatia kilimo bora ili kupata mavuno ya kutosha.
- Sheria ziwekwe za namna ya kuhifadhi na kutunza misitu kwani huvuta mvua.
- Maghala ya kuhifadhi mavuno yajengwe.
- Jamii zinazohamahama zihimizwe kulima na kuweka mifugo wanayoweza kutunza.
- Kukuza zao Fulani maalum katika eneo.
- Wakulima kupewa misaada ya vifaa na mbolea ya kukuza chakula.
- Wakulima kupewa mitaji kutoka kwa serikali.

Sahihi

Nakala kwa:

- Waziri wa kilimo  
Anwani
- Katibu wa kilimo  
Anwani
- Idara husika- anwani

2. Maasi ya vijana yameleta madhara mengi kwa wanafunzi wa shule za upili. Jadili sababu na suluhisho la janga hili.

**a. Visababishi**

- i. Dawa za kulevya
- ii. Shiniko la kikundi/rika.
- iii. Filamu mbaya
- iv. Kudhibitiwa kupita kiasi
- v. Kukosa nidhamu
- vi. Malezi mabaya/udekezaji
- vii. Kubomoka kwa msingi wa jamii
- viii. Ufukara kusababisha kujiunga na makundi haramu
- ix. Kukata tamaa

**b. Suluhisho**

- i. Kujiondoa kundini
- ii. Kuwashauri vijana
- iii. Kujenga udhabiti wa jamii
- iv. Utiifu na unyenyekevu
- v. Kuwa na usemi
- vi. Kuvumiliana na kusameheana
- vii. Kutochagulia watoto taaluma na wachumba
- viii. Wazazi kutolazimisha watoto taaluma au kozi wasizotaka
- ix. Kutopendelea na kulinganisha watoto kiuwezo
- x. Kutotumia dawa za kulevya/hamasisho kuhusu athari za mihadharati
- xi. Kuomba pamoja
- xii. Baba kutimiza majukumu yake ya kukimu jamii
- xiii. Kutodhibiti mke na watoto kupita kiasi
- xiv. Uadilifu

3. Andika kisa kitakachothibitisha ukweli wa methali; Mchelea mwana kulia, hulia yeye.

- **Mtahiniwa aandike kisa kitakachoana na methali hii.**
- **Mwanafunzi azingatie sehemu zote mbili za methali.**

**Maana ya methali**

**Malezi ya kudekeza watoto huleta majuto kwa wazazi baadaye. Mzazi akimdekeza mtoto bila kuwelekeza vyema akiwa na tabia mbaya na kuelekea kuasi bila kumtia adabu, mzazi atakuja kutaabika mwenyewe.**

**TANBIHI**

**Akigusia upande mmoja wa methali atuzwe alama 10**

4. Andika insha itakayomalizia kwa; .....hapo ndipo nilipong'amua kwamba mzazi ni kitu cha thamani.
- **Lazima mtahiniwa amalize kisa kwa maneno aliyopewa; asipomaliza kwa maneno hayo ataadhibiwa kintindo.**
  - **Kisa kiwe cha kusisimua ajabu.**
  - **Mtahiniwa aonyeshe hali ya huzuni (kutendeka kwa jambo la kuhuzunisha)**